



VITUO ATAMIZI VYA PASS AIC, SUA MOROGORO NA TALIRI KONGWA



TANGAZO KWA VIJANA

Kituo cha Ubunifu wa KilimoBiashara (AIC), idara ya Taasisi ya PASS inapenda kuutangazia umma kwamba imefungua milango kwa ajili ya kupokea maombi ya kujiunga na vituo atamizi vya kilimobiashara pale SUA, Morogoro (kilimo cha mbogamboga) na TALIRI, Kongwa (unenepeshaji wa mbuzi).

Vituo atamizi vipo wazi kwa kijana yeyote mwenye sifa na ueledi wa ujasiriamali, elimu, mwenye uzoefu kwenye kilimo na kilimobiashara, awe na tabia njema, utii, nidhamu, mchapa kazi, fikra chanya, mwaminifu na anayependa kuona matokeo chanya. Vijana wa kike wanapewa kipaumbele.

Vijana washiriki kwenye vituo atamizi watapewa vifaa, miundo mbinu, malighali na mtaji wa kufanya kilimobiashara ambapo watausimamia kwa kipindi cha miezi 12. Kwa Kipindi hichi, watapewa usimamizi wa karibu ikiwemo ushauri wa kibiashara na upelembaji ili kuhakikisha wanafanikiwa katika shughuli zao za kilimo biashara. Baada ya muda huo kuisha, vijana watakaofanikiwa kwenye kilimobiashara, PASS AIC watasaidia kufanikisha kuanzisha biashara kama hiyo kwenye eneo la mhitimu kwa kuwezesha kupata mtaji.

Vijana wenye nia wanashauriwa kutuma maombi yao ya kujiunga na vituo atamizi vya PASS AIC. Mchakato wa maombi utajumuisha kujaza fomu ya maombi (inatapatikana kwenye tovuti za AIC na PASS, Kwenye office za PASS, SUA, TALIRI na SUGECO). **Ada ya fomu ni shs 10,000/-.** **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 2/09/2018.** Watakaochagulia watahudhuria mafunzo ya siku 15, ikiwemo siku moja ya kutahiniwa na kuhojiwa. Mchakato wa uchaguzi utafanyika Morogoro na kijana atakayepitia mchakato huu atajikimu kwa gharama zake binafsi na hata baada ya kuchaguliwa kujiunga na vituo atamizi.

Fomu za maombi zinapatikana www.aic.co.tz, www.pass.or.tz